

## **Smittestopp ni nini?**

Smittestopp ni programu kutoka kwa Taasisi ya Afya ya Umma ya Norwe (Norwegian Institute of Public Health (NIPH)). Imeundwa ili kusaidia kuzuia usambazaji wa virusi vya korona katika jamii. Ni hiari yako kutumia programu hii.

Ukipimwa na upatikane kuwa una virusi vya korona, unaweza kuwajulisha watu wengine kupidia programu hii. Wataarifiwa kuwa huenda wameambukizwa virusi vya korona na kupewa ushauri kuhusu hatua ya kuchukua. Kwa kufanya hivyo, programu hii inaweza kuwazuia watu wengi hata zaidi kutoambukizwa virusi vya korona. Programu hii haimwarifu mtu yejote kuwa umeambukizwa virusi vya korona.

## **Ninawezaje kuweka programu ya Smittestopp kwenye simu yangu?**

- Pakua programu kwenye Duka la Programu (App Store) au Google Play.
- Kwenye programu, fuata maagizo yaliyo kwenye skrini.
- Ikiwa huelewi kilichoandikwa, mwombe mtu akufafanulie.

## **Programu ya Smittestopp hufanya kazi vipi?**

Ukiwa karibu na mtu ambaye pia amesakinisha programu kwenye simu yake, simu zitatumiana ishara.

Ikiwa mtu mwingine atapatikana kuwa ana virusi vya korona, programu itakumbuka kuwa simu yako ilikaribiana na mtu huyo aliyeambukizwa virusi vya korona. Kisha, utapokea arifa kupidia programu ikikufahamisha hatua unayopaswa kuchukua.

Unaweza pia kuamua iwapo ungependa kuwaarifu watu wengine ikiwa umeambukizwa virusi vya korona.

Ukipokea ujumbe kupidia programu hii, utafahamishwa tu kuwa ulikaribiana na mtu aliyeambukizwa virusi vya korona wala hutafahamishwa kuhusu mtu aliyeambukizwa virusi vya korona au mahali ulipokaribiana na mtu aliyeambukizwa virusi vya korona. Hakuna yejote iwe ni maofisa wa umma wala mtu binafsi atakayekutambua wala kutambua mahali ulipotembelea.

## **Faragha**

- Ni lazima uwe na umri wa zaidi ya miaka 16 ili utumie programu ya Smittestopp.
- Data inayokuhusu itafutwa baada ya siku 14 bila wewe kuhitaji kuchukua hatua yoyote.
- Unaweza kufuta data inayokuhusu kwenye programu wakati wowote.
- Unaweza kuondoa programu wakati wowote.

## **Jiunge katika mchakato wa kurejesha maisha ya kawaida**

